

## 15- Utekelezaji wa 'Umrah

Endelea kutamka *Talbiyah* ukiwa safarini hadi ufike Masjid Al-Haraam kwa ajili ya kutekeleza taratibu zilobakia za 'Umrah. Ikiwa una mizigo unayohitaji kuiweka hotelini, fanya hivyo. Unaweza kwenda msalani kufanya haja ndogo au kubwa, ukafanya wudhuu, unaweza kula ikiwa umebanwa na njaa. Lakini inapendekezwa kukimbilia kumaliza taratibu za 'Umrah.

### Aina za Twawaaf

**Tanbihi:** Sehemu za kutufu zimeongezwa kwa kuwekwa daraja juu kwa sababu ya upanuzi wa Haram, na ni bora zaidi kutufu huko kwa sababu utaweza kutufu kwa sahali kabisa bila ya msongamano na watu na utasaidia kupunguza zahma katika *Twawaaf* ya ardhini, wala haibadili lolote katika kutekeleza kwake wala haiathiri lolote katika kupata thawabu zake. Kwa miaka ijayo hali itakuwa hivyo hadi upanuzi wa Masjid Al-Haraam umalizike ambao sehemu za kutekeleza *Twawaaf* itazidishwa kiasi kikubwa kuweko mizunguko kadhaa ili iwatosheleze watu.

- **Twawaaf Al-'Umrah:** Ni nguzo mojawapo ya 'Umrah. Ni *Twawaaf* inayotekelezwa na kila aliyeingia Ihraam kwa ajili ya kutekeleza 'Umrah.
- **Twawaaf Al-Quduwm:** Ni *Twawaaf* inayotekelezwa na aliyeingia Ihraam kwa ajili ya kutekeleza Hajj ya *Qiraan* au *Ifraad* nayo ni Sunnah kama walivyokubaliana Wanachuoni. Kwa hiyo kuachwa kwake haibatilishi Hajj, lakini inapendekeza kutekelezwa. Ama madhehebu ya Imaam Maalik ni waajib kwa kuwa kachukua dalili ya kauli ya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipoelekea *Al-Ka'bah* akasema: **((Chukueni kutoka kwangu manaasik zenu)).<sup>1</sup>**
- **Twawaaf Al-Ifaadhwah:** Ni *Twawaaf* inayowapasa Mahujaji wa aina zote za Hajj kutekeleza pindi watakapomaliza kusimama 'Arafah na kukesha *Muzdalifah*. Nayo ni nguzo mojawapo ya Hajj, kuiacha kutekeleza, Hajj haitimii.
- **Twawaaf Al-Wadaa'i:** Ni *Twawaaf* ya kuaga inayotekelezwa mwisho kabisa baada ya kumaliza Umrah au Hajj, nayo iwe ni 'amali yako ya mwisho kabla ya kuondoka Makkah. Wanachuoni wamekubaliana

---

<sup>1</sup> Muslim.

kwamba hukmu yake ni waajib kwa hiyo atakayeacha kutekeleza atawajibika kufanya *kaffaarah* ya kuchinja. Ama wanawake wenye hedhi au nifaas wao wameruhusika nayo.

- **Twawaaf At-Tatwawwu'**: *Twawaaf* inayotekelezwa akipenda mtu anapoingia Masjid Al-Haraam kisha aswali rakaa mbili Maqaam Ibraahiyim au popote pale.

### Ya kutekeleza unapofika Masjid Al-Haraam

- Mahujaji anapoingia Msikitini atangulize mguu wake wa kulia na kusoma du'aa ya kuingia Masjid:

أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ، وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ، وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ، مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، (بِسْمِ اللَّهِ،  
وَالصَّلَاةِ) (وَالسَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ)، اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ

**A'uwduhu biLlaahil-'Adhwiym, wabi Wajhihil-Kariym wa-Sultwaanihil-qadiym, minash-shaytwaanir-rajiym (BismiLlaah was-swalaatu) (was-salaamu 'alaa Rasuwli-Llaah) Allaahummaftah-liy abwaaba Rahmatika**

"Najikinga na Allaah Mtukufu, na kwa Wajih Wake Mkarimu, na kwa utawala Wake wa kale, dhidi ya shaytwaan aliyeepushwa na Rahmah za Allaah (Kwa jina la Allaah na Rahmah na amani zimfikie Rasuli wa Allaah) Ee Allaah nifungulie milango ya Rahmah Yako."

- Niyyah iwekwe moyoni ya aina *Twawaaf* unayotekeleza.
- Anza *Twawaaf* katika *Al-Hajar Al-As-wad*. Libusu ukiweza kupata nafasi na dalili ni Hadiyth ya 'Umar bin Khatwaab (رضي الله عنه) kwamba alilifikia *Al-Hajar Al-As-wad* akalibusu kisha akasema:

"إِنِّي أَعْلَمُ أَنَّكَ حَجَرٌ لَا تَضُرُّ وَلَا تَنْفَعُ، وَلَوْلَا أَنِّي رَأَيْتَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يُقْبَلُكَ  
مَا قَبَّلْتُكَ" - البخاري و مسلم

“Hakika mimi najua kwamba wewe ni jiwe usiloweza kudhuru wala kunufaisha, na ingelikuwa sikumuona Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم) anakubusu basi nami nisingelikubusu.”

- Ikiwa kuna zahma, haipasi kabisa kusukumana na watu kwa ajili ya kubusu *Al-Hajar Al-As-wad*, inatosheleza kulielekea hata ukiwa mbali kisha nyanyua mkono wako wa kulia kuliashiria (*istilaam*) useme:

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُ أَكْبَرُ

**BismiLLaah, Allaahu Akbar**

Kwa Jina la Allaah, Allaah ni Mkubwa.

**Tanbihi:** Usibusu mkono wako kwani si katika Sunnah!

- Utaanza kutufu *Al-Ka'bah* kuanzia pembe ya *Al-Hajar Al-As-wad*.
- Lazima utembe huku *Al-Ka'bah* liko kushotoni mwako. Unapofika *Rukn Al-Yamaaniy* uiguse lakini usibusu. Na utakapokuwa baina yake na *Al-Hajar Al-As-wad* useme:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

**Rabbanaa Aatinaa fid-dun-yaa hasanataw-wafil- Aakhirati hasanataw-waqinaa 'adhaaban-Naar.**

“Rabb wetu Tupe katika dunia mema na katika Aakhirah [pia Tupe] mema na Tukinge na adhabu ya Moto.”<sup>2</sup>

- Kila mara ukilipita *Al-Hajar Al-As-wad* kuanza mzunguko wa pili na kuendelea, unatakiwa useme “*Allaahu Akbar*” huku ukiwa umenyanyua mkono wako wa kulia na kuliashiria, na bila ya kutanguliza kusema ‘*BismiLLaah*’.
- Katika kufanya *Twawaaf* zilizobakia unaweza kusema unachopenda katika dhikru-Allaah; kusoma Qur-aan, kuleta *Istighfaar*, *du'aa*,

---

<sup>2</sup> Al-Baqarah (2: 201).

*tasbiyh, tahliyl, tahmiyd, takbiyr, kumswalia* Nabiyy (صلى الله عليه وآله وسلم). Hii kwa sababu *Twawaaf, As-Sa'-y* na *Jamaraat* imehusishwa kwa ajili ya kumdhukuru Allaah.

- Katika *Twawaaf* hii wanaume wanahitajia wafanye vitu viwili:
- i. Uweke *Al-Idhwtwibaa'* kutoka mwanzo wa *Twawaaf* mpaka mwisho. *Al-Idhwtwibaa'* ina maana kwamba ni kuweka sehemu ya katikati ya vazi (ridaa) chini ya kwapa lako la kulia na kipande cha ridaa akipitisha juu ya bega la mkono wa kushoto. Unapomaliza kufanya *Twawaaf* unaweza kurudisha ridaa yako katika hali yake ya mwanzo kwa sababu wakati wa *Idhwtwibaa'* ni wakati wa *Twawaaf* tu.
  - ii. Kufanya *Ar-Raml* katika *Twawaaf* tatu za mwanzo. *Ar-Raml* ina maana kwamba kuzunguka kwa mwendo wa haraka kwa hatua ndogo ndogo. Kisha unatakiwa utembe mwendo wa kawaida katika *Twawaaf* zako nne za mwisho, na dalili yake ni Hadiyith ya Jaabir (رضي الله عنه)

"أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَمَّا قَدِمَ مَكَّةَ أَتَى الْحُجَرَ فَاسْتَلَمَهُ ثُمَّ مَشَى عَلَى يَمِينِهِ فَرَمَلَ ثَلَاثًا وَمَشَى أَرْبَعًا" - مسلم

"Rasuli wa Allaah alipofika Makkah alilifikia *Al-Hajar Al-As-wad* akaliashiria kisha akatembea kuliani mwake akafanya *Ar-Raml* mizunguko mitatu na akatembea (kikawaida) mizunguko minne."<sup>3</sup>

## Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa

- Kuanza *Twawaaf* katika chanzo kingine kisichokuwa sehemu ya *Al-Hajar Al-As-wad* na hali ni fardhi kuanzia *Twawaaf* hapo.

---

<sup>3</sup> Muslim.

- Kutufu ndani ya eneo la Hijr kutokana na msongamano mkubwa wa watu. Kimsingi hili ni kosa kubwa kwa sababu kishariy'ah, eneo la Hijr liko ndani ya *Al-Ka'bah* na *Twawaaf* inatakiwa iwe nje ya *Al-Ka'bah* na sio ndani ya *Al-Ka'bah*. Kwa hiyo kwa kupita ndani ya Hijr unapotufu unakuwa umetufu katika sehemu ya *Al-Ka'bah* na si *Al-Ka'bah* yote ambayo ndiyo inayotakiwa.
- Kufanya *Ar-Raml* katika *Twawaaf* zote saba na hali *Ar-Raml* inatakikana kufanywa katika mizunguko mitatu tu ya mwanzo.
- Kusukumana na watu na kusababisha zahma, kuwaumiza watu kutaka kulifikia *Al-Hajar Al-As-wad* ili kulibusu. Vitendo kama hivi vinaleta madhara kwa Waislamu na haturuhusiwi kufanya hivyo. Itambulike kuwa *Twawaaf* inabakia kuwa sahihi bila ya kulibusu *Al-Hajar Al-As-wad*.
- Kubusu mkono baada ya kuashiria *Al-Hajar Al-As-wad* unapokuwa mbali nalo, kwani ni kinyume na Sunnah.
- Mahujaji kufuta au kusugua mkono wake katika *Al-Hajar Al-As-wad* akitegemea kupata baraka. Hili ni jambo lisilokuwa na dalili katika shariy'ah ya Kiislam, hivyo ni bid'ah na shirki. Sunnah ni kuligusa tu au kulibusu inapokuweco uwezekano wa kufanya hivyo bila ya tabu yoyote.
- Kugusa pembe nne za *Al-Ka'bah* au kuta zake, kusugua na kujipangusa nayo kwa kutegemea kupata baraka. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakugusa sehemu yoyote ya *Al-Ka'bah* isipokuwa *Al-Hajar Al-As-wad* na *Ar-Ruknul-Yamaaniy*.
- Kusoma du'aa zilizotajwa kuwa ni maalumu kwa kila *Twawaaf* moja. Utakuta kuna vijitabu vidogo vidogo vinauzwa vyenye du'aa maalum kwa kila *Twawaaf*. Vitabu hivyo havina mashiko. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) hakueleza bayana du'aa yoyote isipokuwa ni kusema 'Allaahu Akbar' anapofikia *Al-Hajar Al-As-wad* na kila anapomaliza *Twawaaf* moja baina ya *Ar-Ruknul-Yamaaniy* na *Al-Hajar Al-As-wad* akisoma du'aa iliyotajwa juu. Amesema Shaykhul Islaam Ibn Taymiyah (رحمه الله): "Hakuna katika kutufu dhikri au du'aa maalumu

kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم); si kwa amri yake wala kauli yake wala mafunzo yake, bali anachotakiwa mtu ni kuomba du'aa mbalimbali na kile kitajwacho na watu wengi kuwa kuna du'aa maalumu za kuzungukia Al-Ka'bah hilo halikuthibiti kutoka kwa Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم).

- Kupandisha sauti ya anayeongoza watu kutufu na wale wanaoongozwa katika hizo du'aa ambazo watu wamejipangia. Kufanya hivyo kunasababisha kubabaisha Mahujaji wengine wanaomdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) kwa pole pole na wanawakosesha *khushuu'*. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى): **((Muombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa khofu, hakika Yeye Hapendi wavukao mipaka)).**<sup>4</sup>
- Kusimama kuomba du'aa baada ya kumaliza *Twawaaf*.

### **Maqaam Ibraahiym**

- Utakapomaliza mizunguko saba ya *Twawaaf*, utakaribia Maqaam Ibraahiym na utasoma:

﴿وَأَتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى﴾

**((Na chukueni kutoka mahali pa kusimama Ibraahiym kuwa ni pahala pa kuswalia)).**<sup>5</sup>

- Utaswali rakaa mbili fupi, ukiwa karibu kiasi iwezekanavyo na nyuma ya Maqaam Ibraahiym. Katika rakaa ya mwanzo utasoma Suratul-Kaafiruw (Qul yaa ayyuhal-kaafiruw) na rakaa ya pili utasoma Suratul-Ikhlaasw (Qul-Huwa-Allaahu Ahad) baada ya kuisoma Suratul Faatihah katika kila rakaa.
- Utakapomaliza rakaa mbili, ni Sunnah kuelekea kwenye mifereji ya Zamzam kunywa maji yake. Unapokunywa omba du'aa unayotaka

---

<sup>4</sup> Al-A'raaf (7: 55).

<sup>5</sup> Al-Baqarah (2: 125).

kwani kwa kuyanywa du'aa hutakabaliwa kama alivyosema Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

((مَاءٌ زَمْزَمٌ لِمَا شُرِبَ لَهُ))

**((Maji ya Zamzam kwa (jambo liloombewa) wakati wa kunywa)).<sup>6</sup>**

- Utarudi kuligusa *Al-Hajar Al-As-wad* kama itawezekana. Ikiwa kuna zahma basi hakuna lazima kufanya, bali ni makosa kuingia kusababisha msukumano na watu.

### **Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kujilazimisha kuswali karibu na Maqaam Ibraahiym kunapokuwa kuna zahma za watu. Hivi husababisha maudhi na misongamano ambayo huishia kuumizana na Mahujaji wengine. Inatosheleza kuswali rakaa mbili baada ya kumaliza *Twawaaf* mahali popote nyuma ya Maqaam hata kwa mbali na ikiwa ni zahma hapo basi popote pale katika Masjid Al-Haraam. Hivi itakuepusha kuudhi watu na kuudhiwa na watu na utaweza kuswali kwa unyenyekevu zaidi na utulivu.
- Kuswali zaidi ya rakaa mbili na kusababisha zahma na hali watu wanahitaji nao kutimiza hizo rakaa mbili na mahali panakuwa pa dhiki mno.

---

<sup>6</sup> Ibn Maajah, Ahmad na Al-Albaanyi ameipa daraja ya Swahiyh katika Swahiyh Ibn Maajah.



## Taratibu Za Kutekeleza Twawaaf Kwa Mukhtasari



### Asw-Swafaa Na Al-Mar-wah

- Utakwenda Al-Mas-'aa, utakapofika karibu na Asw-Swafaa utasoma:

﴿ إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ﴾



**((Hakika Asw-Swafaa na Al-Mar-wah ni katika alama za [Dini ya Allaah]).<sup>7</sup>**

- Utapanda (kilima cha) Asw-Swafaa mpaka uweze kuona Al-Ka'bah (ikiwezekana). Elekea Al-Ka'bah na nyanyua mikono yako, umtukuze Allaah na useme ifuatavyo kisha uombe du'aa upendayo:

لا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ أَجْزَأُ وَعَدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ

**Laa Ilaaha Illa-Allaah Wahdahu laa shariyka Lahu, Lahul-Mulku Walahul-Hamdu wa Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr. Laa Ilaaha Illa-Allaahu Wahdahu, Anjaza wa'dahu wa-Naswara 'Abdahu wa-hazamal-ahzaaba Wahdahu**

“Hapana ilaah (muabudiwa wa haki) ila Allaah, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na ni Zake sifa njema Naye juu ya kila kitu ni Muweza. Hapana ilaah ila Allaah, hali ya kuwa Peke Yake, Ametekeleza ahadi Yake, na Amemnusuru mja Wake, na Amevishinda vikosi peke Yake.”

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisoma hivi mara tatu na baina yake akiomba du'aa, kisha akafanya alipokuwa Al-Mar-wah kama alivyofanya alipokuwa Asw-Swafaa<sup>8</sup>.

- Kisha teremka Asw-Swafaa na elekea Al-Mar-wah kwa mwendo wa kawaida mpaka unapofika katika alama ya taa za kijani utafanya Ar-Rakdhw. Alama ya kijani inadhihirika juu ya sakafu kwa taa rangi ya kijani. Hapo utakwenda mwendo wa kukimbia mpaka alama hiyo ya taa za kijani zinapomalizikia. Wanawake hawatakiwi kufanya Ar-Rakdhw. Endelea kuelekea Al-Mar-wah kwa mwendo wa kawaida. Utakapofikia kilima na kuelekea Qiblah, nyanyua mikono na kurudia kusema kama ulivyosema ulipokuwa Asw-Swafaa. Kisha teremka Al-

---

<sup>7</sup> Al-Baqarah (2:158).

<sup>8</sup> Muslim (2/8880).

Mar-wah kuelekea Asw-Swafaa, ukihakikisha unatembea sehemu zinazohusika na kukimbia katika sehemu zinazohusika.

- Eendelea kufanya hivyo mpaka umalize mizunguko saba. Kutoka Asw-Swafaa kwenda Al-Mar-wah ni mzunguko mmoja na kurudi ni mzunguko mwengine. Unatakiwa kumdhukuru Allaah (سبحانه وتعالى) wakati wote wa As-Sa'-y kwa kusoma au kusema unachopenda; Qur'aan, du'aa, Istighfaar, tasbiyh, tahliyl, tahmiyd, takbiyr, kumswalia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) n.k.
- Utakapomaliza As-Sa'-y utanyoa nywele. Mwanamke utakata nywele kiasi cha urefu wa ncha ya kidole. Kwa wanaume, inapendekezeka kunyoa nywele zote, na kunyoa ni bora kuliko kukata kwani Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwaomba du'aa Maswahaba walionyoya mara tatu na waliokata mara moja kwa dalili Hadiyth ya 'Abdullaah bin 'Umar (رضي الله عنه) kwamba Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisema:

((رَحِمَ اللهُ الْمَخْلِقِينَ)) قالوا: والمقصِّرينَ يا رسولَ اللهِ؟ قال: ((رَحِمَ اللهُ الْمَخْلِقِينَ)) قالوا: والمقصِّرينَ

يا رسولَ اللهِ؟ قال: ((رَحِمَ اللهُ الْمَخْلِقِينَ)) قالوا: والمقصِّرينَ يا رسولَ اللهِ؟ قال: ((والمقصِّرينَ))

مسلم وغيرهم

**((Allaah Awarehemu walionyoa))** Wakauliza: “Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?” Akasema: **((Allaah Awarehemu walionyoa))** Wakauliza: “Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?” Akasema: **((Allaah Awarehemu walionyoa))** Wakauliza: “Na waliopunguza ee Rasuli wa Allaah?” Akasema: **((Na waliopunguza)).<sup>9</sup>**

Isipokuwa ikiwa tarehe 8 ya Hajj iko karibu na hakuna wakati wa kutosha kwa nywele kurudi kukua, basi ni bora kukata ili nywele zibakie kwa ajili ya kunyoa baada ya kulala Muzdalifah, kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwaamrisha Maswahaba kukata nywele katika 'Umrah kwani walifanya asubuhi ya tarehe nne ya Dhul-Hijjah.

---

<sup>9</sup> Muslim na wengineo kwa maelezo tofauti kidogo.

- Baada ya hapo 'Umrah itakuwa imemalizika na utakuwa huru kuvaa nguo nyingine, kutia manukato (mwanamume) na kurudia hali ya ndoa (kujimai) na kadhalika.

### **Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kwenye kupanda kilima cha *Asw-Swafaa* na *Al-Mar-wah*, baadhi ya Mahujaji wanaelekea *Al-Ka'bah* na kuiashiria kwa mikono wakisema '*Allaahu Akbar*' kama vile wanavyosema *takbiyrah* ya Swalaah. Kuashiria hivyo ni makosa kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alinyanyua mikono yake kumdhukuru Allaaah na komba du'aa pekee.
- Kufanya *Ar-Rakdhw* katika masafa yote baina ya vilima viwili. Sunnah ni kuchapuzwa mwendo baina ya alama zilowekwa za taa ya kijani sakafuni na kutembea mwendo wa kawaida kwengine kote.
- Wanawake kufanya *Ar-Rakdhw* kwani *Ar-Rakdhw* ni kwa ajili ya wanaume pekee.
- Kusoma adhkaar kwa pamoja akiwa mtu mmoja anaongoza wenziwe. Ni makosa makubwa kufanya hivi kwani inasababisha zahma za magurupu ya watu kutembea pamoja na sauti moja na kuwabababisha Mahujaji wengineo katika adhkaar zao.
- Kuleta mazungumzo wakati wa *As-Sa'-y* na hali hapo ni mahali pa kumdhukuru Allaaah (سبحانه وتعالى).

